# JARIDA LA MTANDAO TIA









# UTEKELEZAJI WA MRADI WA HEET TAASISI YA UHASIBU TANZANIA (TIA)



**UTANGULIZI**

Mradi wa Mageuzi ya Kiuchumi kwa vyuo vya Elimu ya Juu (Higher Education Economic Transformation-HEET) ni mradi unaotekelezwa chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MOeST) kupitia benki ya Dunia (World Bank). Lengo la mradi huu ni 'Kuimarisha mazingira ya kujifunzia na kufundishia ili kuendana na soko la ajira katika programu za kipaumbele katika taasisi za elimu ya juu na kuboresha mfumo wa usimamizi wa elimu ya juu'."

Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) ni kati ya Taasisi zinazotekeleza mradi huu wa HEET. Mradi huu unatekelezwa kwa muda wa miaka mitano (5) na unatekelezwa katika Kampasi ya Mwanza na Singida kwa potfolio namba 1 ya ujenzi na ukarabati. Taasisi imetengewa kiasi cha takriban Bill 27.6 za kitanzania. Utekelezaji wa mradi huu umejikita katika maeneo saba (7) ambayo ni

i. Ujenzi na ukarabati wa miundombinu.
ii. Uboreshaji wa mitaala na mbinu bunifu za ufundishaji.
iii. Kukuza utafiti wa vitendo na ubunifu;
iv. Kujenga uhusiano madhubuti na sekta binafsi/viwanda.
v. Kuimarisha matumizi ya teknolojia ya kidijitali.
vi. Kukuza mapato yanayozalishwa ndani ya Taasisi.
vii. Kujengea uwezo wa wafanyakazi na Viongozi.

**KARIBU UPATE MATUKIO MBALIMBALI YALIYOJIRI KATIKA UTEKELEZAJI WA MALENGO HAYA 7.**

# 1 TIA YAZINDUA KAMATI YA USHAURI WA KITASNIA

Na Gloria Mwakilave
Dar es Salaam




Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha Bi. Amina K. Shaaban alizindua rasmi Kamati ya Ushauri ya Kitasnia chini ya Mradi wa HEET ambayo itaenda kuwa kiungo muhimu katika kuimarisha uhusiano kati ya Taasisi na wadau mbalimbali wa sekta binafsi

Wakati akizindua Kamati hiyo kwenye hafla fupi iliyofanyika Ukumbi wa TIA, Naibu Katibu Mkuu alisema Kamati hiyo itakuwa na mchango mkubwa katika uhuishaji na uandaaji wa mitaala itakayokidhi soko la ajira na kuhakikisha mazingira bora ya kujifunzia yanapatikana.

Aidha, Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania Profesa William Pallangyo alisema TIA inatimiza adhma ya Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuhakikisha kuna mahusiano ya karibu kati ya taasisi za elimu ya juu na sekta binafsi katika utoaji mafunzo, utafiti, na ushauri wa kitaalamu.

“TIA tunatambua kwamba Mradi wa HEET una lengo kuu la kuimarisha mazingira ya kujifunzia na muelekeo wa soko la ajira katika vipaumbele vya programu za taaluma na usimamizi wa mfumo wa elimu ya juu,”. Alisema Profesa Pallangyo

Pia, Mratibu wa Mradi wa HEET TIA Ndg. Oyombe Simba alisema katika utekelezaji wa mradi huu, TIA imetengewa dola za Marekani Milioni 11.7 ambazo ni sawa na shilingi za kitanzania Bill 27.6 ili kugharamia shughuli za mradi kama ilivyopitishwa katika mpango mkakati wa uwekezaji wa Taasisi,

“Fedha hizo zimetengwa ili kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa Hosteli za Kike na Kiume Kampasi ya Mwanza, kuongeza miundombinu ya kujifunzia kwa Kampasi ya Singida” Alisema Simba

Prof. Mussa J. Assad ambaye ni mhadhiri wa Chuo Kikuu Muslim Morogoro na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Mstaafu na Mwenyekiti wa kamati hiyo alishukuru Serikali kwa kuchukulia kwa uzito suala la uhuishaji wa mitaala mipya ambayo itaendana na soko la ajira la kimataifa na mabadiliko ya kiteknolojia,

“Nawashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati hii kwa kukubali kushirikiana na TIA katika kutekeleza jukumu hili kubwa,”. Alisema Profesa Assad










# WARATIBU WA MRADI WA HEET TAIFA WATEMBELEA TIA

Na Beatrice Njokamtaly
Dar es Salaam

Waratibu wa mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi ( HEET) Taifa walitembelea Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) na kufanya kikao cha pamoja cha ufuatiliaji wa maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo, ikiwa TIA ni moja ya wanufaika wa mradi wa HEET unaofadhiliwa na Serikali kupitia Benki kuu ya dunia.



Akitoa Taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, Mratibu wa mradi wa TIA Oyombe Simba alisema TIA inaendelea kutekeleza mradi huo kwa kasi, kwa kuanzia kuwajengea uwezo Maafisa TEHAMA, kuhuisha na kuunda mitaala 6 ya Shahada ya kwanza na Shahada ya Uzamili.

Pia Mratibu Oyombe alisema mradi wa HEET umetoa fursa kwa wahadhiri wanawake watatu kusoma Shahada ya juu ya Uzamivu, mafunzo ya mabadiliko ya Uongozi kwa Viongozi Wakuu wa Taasisi pamoja na kuwajengea uwezo waratibu wa mradi wa TIA katika masuala ya Mikataba.



Kwa upande wa Miundombinu Mratibu alisema tayari maandilizi ya awali yamefanyika katika Ujenzi wa jengo la  kitaaluma Kampasi ya Singida na mabweni Kampasi ya Mwanza , na inatarajiwa kuanza ujenzi mapema  2024.

3

# KAMATI ZA MASHAURIANO YA KITASNIA ZANOLEWA NA MRADI WA HEET







Na Beatrice Njokamtaly
Dar es Salaam

Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia imeandaa kikao cha kitaifa cha Kamati za Ushauri za Kitasnia (Industrial Advisory Committees) kwa lengo la kuongeza ufanisi wa vyuo vya elimu ya juu katika kuchangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET).

Kikao hicho kilifanyika katika Ukumbi wa Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kikihusisha kamati kutoka vyuo mbalimbali vya elimu ya juu vinavyonufaika na mradi wa HEET. Washiriki walijadili njia za kuboresha ushirikiano kati ya taasisi za elimu ya juu na sekta binafsi, huku wakilenga kuongeza ubunifu, tafiti, na mitaala yenye tija.

Miongoni mwa vyuo vilivyoshiriki ni Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA). Wajumbe wa TIA walihudhuria mafunzo yaliyolenga kuboresha programu zao ili ziendane na mahitaji ya soko la ajira.

Kwa mujibu wa Dkt. Kasambala, Naibu Makamu wa Chuo Taaluma, Tafiti na Ushauri wa Kitaalam, “Kamati hizi zinatoa jukwaa la kubuni mitaala mipya na kuboresha iliyopo. Lengo ni kuhakikisha vijana wanakuwa na ujuzi wa kidijitali na uwezo wa kushughulikia changamoto za kiuchumi na kijamii,” alisisitiza Dkt. Kasambala.

Dkt. Elimeleck Akyoo, Mratibu wa Ushauri wa Kitasnia wa TIA na Katibu wa Kamati hiyo ya Mashauriano, aliongeza kuwa, “Kazi ya kamati hizi ni kuleta taarifa sahihi kuhusu mahitaji ya soko la ajira na kusaidia vyuo kutengeneza mipango madhubuti ya maendeleo,” alisisitiza Dkt. Akyoo.

Washiriki walipongeza mradi wa HEET kwa kuanzisha kamati hizi, wakisema zitaimarisha tafiti na bunifu zenye tija kwa vijana wa sasa na kizazi kijacho.

# 4 TIA IMEANDAA SERA YA MAKUNDI MAALUMU KATIKA UTOAJI HUDUMA









Na Gloria Mwakilave
Morogoro

Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA), Profesa William Pallangyo, alisisitiza umuhimu wa taasisi kuwa na sera inayotoa mwongozo wa namna walengwa wa mahitaji maalumu watakavyohudumiwa. Alieleza kuwa sera hiyo inapaswa kuzingatia aina ya miundombinu ya utoaji wa huduma za elimu kwa wanafunzi na wafanyakazi.

Kauli hiyo aliitoa alipofungua kikao kazi cha kuandaa sera ya Watu wenye Mahitaji Maalumu (Special Needs Policy) na sheria za kazi, kilichofanyika katika ukumbi wa Kigurunyembe, Morogoro.

Aidha, kikao hicho kilihusiana na mradi wa ujenzi wa kampasi za Singida na Mwanza, unaotekelezwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia mradi wa mabadiliko ya kiuchumi kwa elimu ya juu (HEET),

"Nasisitiza kwamba, wakati wa maandalizi ya sera hizi, inahitajika kuzingatia mahitaji maalumu ya makundi mbalimbali. Sera hizi zizingatie usawa na kuhakikisha upatikanaji wa huduma kwa wote. Pia, maandalizi hayo yawahusishe watu wa ndani na nje ya TIA, pamoja na kutumia tafiti na takwimu za kutosha,". alisema Profesa Pallangyo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Huduma za Wanachuo na Mratibu wa Makundi Maalumu wa mradi wa HEET, Lucina Comino, alisema sera hiyo ililenga kutoa mwongozo wa maandalizi ya mitaala, mbinu na vifaa vya kufundishia, utungaji wa mitihani, uchapishaji wa mitihani, ufanyaji wa mitihani, usahihishaji, na utoaji wa matokeo kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu,

"Sera hii inalenga kuhakikisha kuwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu wanapata huduma bora na zenye usawa kama wenzao,". alisema Comino.

Kikao kazi hicho kilifadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia mradi wa HEET, ambapo TIA ni moja ya taasisi zilizotekeleza mradi huo.




# TIA YAJENGEA UWEZO WANATAALUMA KATIKA UUNDAJI NA UHUISHAJI WA MITAALA

Na Andrew Ntobi

Morogoro

Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA), kupitia ufadhili wa Mradi wa Higher Education for Economic Transformation (HEET), iliendesha mafunzo maalum kwa wahadhiri wake kuhusu uundaji wa mitaala mipya na uhuishaji wa mitaala iliyokuwa ikitumika.

Mafunzo hayo yaliwalenga watumishi walioshiriki katika mchakato wa kubuni na kuboresha mitaala sita (6) iliyotarajiwa kuendana na mahitaji ya soko la ajira.

Lengo kuu la mafunzo hayo lilikuwa kuwajengea uwezo wanataaluma katika kubuni mitaala iliyowawezesha vijana kuwa na umahiri wa kujiajiri, kuajirika, na kutumia teknolojia za kisasa, hususan TEHAMA.

Aidha, mitaala hiyo ililenga kukuza weledi wa wanafunzi kwa kuzingatia mahitaji ya waajiri na sekta mbalimbali.

Katika mafunzo hayo, umuhimu wa kushirikisha wadau mbalimbali, ikiwemo waajiri na taasisi za elimu, ulisisitizwa ili kuhakikisha ubora wa mitaala iliyoundwa. Ushirikiano huo ulitarajiwa kuwezesha TIA kuzalisha wahitimu waliolingana na mahitaji ya soko la ajira la wakati huo.

Chini ya mradi wa HEET, TIA pia ilikuwa imeweka mkakati wa kuhakikisha mitaala yake ilizingatia masuala ya kijinsia na mahitaji ya makundi maalum. Vifaa, mbinu za ufundishaji, na mazingira ya kujifunzia yalitarajiwa kuwiana na mahitaji ya wanafunzi wote bila ubaguzi.

Kupitia hatua hiyo, TIA ilithibitisha dhamira yake ya kutoa elimu bora na mitaala yenye ubunifu na tija kwa maendeleo ya kiuchumi.







# WANANCHI WA MWANZA NA SINGIDA WAPEWA ELIMU YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA HEET

Na Andrew Ntobi
Singida





Waratibu wa masuala ya Jamii katika utekelezaji wa mradi wa HEET unaoendelea kwa Kampasi za Mwanza na Singida wametoa elimu ya mradi wa HEET katika kipindi chote cha utekelezaji huo.

Mratibu Sofia Venance amesema kipindi cha utekelezaji wa mradi ni muhimu wananchi kufahamu namna mradi utaavyotelezwa, jinsi malalamiko yatakavyoshughulikiwa na fursa zilizopo katika maeneo yanayozunguka miradi,

“Nawasihi tujiepushe na vishawishi vya wageni wa nje wanaokuja kufanya kazi na kuondoka kwa kutokuanzisha mauhusiano ambayo yanaweza pelekea ukapata mtoto na baadae ukatekelezwa ,”. Alisisitiza Mratibu Sofia

Naye, Mratibu Simon Wankogere amesema miradi hii inayotekelezwa na Serikali ya awamu ya sita imelenga kutekelezwa bila kuathiri mazingira na endapo kutakuwa na changamoto yoyote ya kimazingira basi wananchi wasisite kutoa taarifa katika ofisi ya malalamiko ili kupatiwa ufumbuzi.

“Ukiona mkarandasi hajafuata sheria za usalama mahala pa kazi,vibarua hawajalipwa, au changamoto yoyote ambayo inaweza kwamisha maendeleo ya utekelezaji wa mradi basi usisite kutoa taarifa,”. Alisisitiza Mratibu Simon

# 7 BILIONI 7.2 KUJENGA MABWENI MAWILI KAMPASI YA TIA MWANZA CHINI YA MRADI WA HEET






Na Gloria Mwakilave
Mwanza

Mkuu wa Wilaya ya Misungwi, Mhe. Johari Samizi, aliwaagiza wananchi wa mtaa wa Nyanghomango kulinda miundombinu ya ujenzi wa mabweni ya wanafunzi katika Taasisi ya Uhasibu Tanzania Kampasi ya Mwanza, mradi utakaogharimu shilingi bilioni 7.2.

"Mradi wa ujenzi huu ni kazi kubwa inayofanywa na Serikali ya awamu ya sita, chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, lazima tuitunze na kuilinda,. Alisisitiza DC Johari.

Alizungumza hayo Oktoba 17, 2024, wakati wa hafla ya kukabidhiana hati za ujenzi wa mabweni mawili baina ya kampuni ya Wakandarasi ya CAIEC (International) na Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA), wenye thamani ya Shilingi bilioni 7.2, wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 306, wakiwemo wa kike na wa kiume.

Afisa Mtendaji Mkuu wa TIA, Profesa William Pallangyo, alisisitiza kuwa mkandarasi CAIEC International lazima akamilishe ujenzi huo kwa wakati kama ambavyo walikubaliana kwenye mkataba wa makubaliano wa kazi.


"Fedha hizi zimetolewa na Serikali chini ya mradi wa HEET kupitia Benki ya Dunia, ukilenga kuboresha malazi kwa wanachuo wetu wa kike na wa kiume. Ni matumaini yetu mradi utakamilika kwa wakati na kwa kuzingatia viwango vya hali ya juu,". Alisisitiza Profesa Pallangyo.

Naye, George Moses, msaidizi wa Mkurugenzi wa CAIEC International, alisema watazingatia mkataba wa makubaliano na kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati na viwango vya kimataifa ili kuhakikisha lengo la TIA na Serikali kwa jumla la kuboresha malazi ya wanafunzi linatimia.

Kwa nyakati tofauti, wanachuo walieleza furaha yao kwa Serikali ya awamu ya sita kwa kuboresha miundombinu.

"Tumeona picha namna hosteli zetu zitakavyokuwa baada ya ujenzi, tumefurahi sana,". Walieleza wanachuo.

# TIA YASAINI MKATABA NA SALEM CONSTRUCTION LIMITED KWA UJENZI WA KAMPASI YA SINGIDA




Na Andrew Ntobi
Dar es Salaam

Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA), Profesa William Pallangyo, alisaini mkataba na kampuni ya Salem Construction Limited kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Taaluma katika Kampasi ya Singida.

Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia Mradi wa Higher Education for Economic Transformation (HEET), unaosimamiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Ujenzi huo unakadiriwa kugharimu shilingi bilioni 13.5 na unatarajiwa kukamilika ndani ya miaka miwili.

Akizungumza katika hafla ya kusaini mkataba huo iliyofanyika Makao Makuu ya TIA, Dar es Salaam, Profesa Pallangyo alisisitiza umuhimu wa kuzingatia ubora na usalama katika utekelezaji wa mradi huo,

"Naomba nisisitize Salem Construction kuhakikisha kazi inafanyika kwa viwango vya juu vya ubora, kutoa ajira kwa wakazi wa Singida, na kuzingatia usalama wakati wa ujenzi. Kampasi yetu ya Singida ilikuwa ikikua kwa kasi, na tayari tulikuwa tunatoa shahada ya uzamili. Kukamilika kwa wakati kwa ujenzi huu ni furaha kwa TIA na jamii inayotuzunguka,". alisema Prof. Pallangyo


Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Idara ya Elimu ya Juu na Mratibu wa Mradi wa HEET Taifa, Dkt. Kennedy Hosea, aliipongeza TIA kwa hatua kubwa iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huo,

"Nipende kuwapongeza TIA. Kulikuwa na taasisi nyingi zilizoanza utekelezaji wa miradi kama huu kabla yenu, lakini ninyi mmeweza kupiga hatua kubwa. Salem Construction, tunaomba mzingatie kanuni na sheria za Mradi wa HEET pamoja na taratibu za serikali,". alisema Dkt. Hosea.

Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaaluma, Dkt. Momole Kasambala, aliishukuru Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha utekelezaji wa mradi huo,

"Mradi huu unalenga kuimarisha mazingira ya kujifunzia, na ujenzi wa Jengo la Taaluma katika Kampasi ya Singida ikiwa ni hatua muhimu katika kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu bora,". alisema Dkt. Kasambala

Ujenzi wa Kampasi ya Singida unatarajia kuchochea maendeleo ya elimu na uchumi katika eneo hilo kwa kuongeza nafasi za ajira, kuboresha miundombinu, na kuimarisha ustawi wa jamii.




# BODI YA WAHARIRI

1 - Dkt Issaya Hassanal -Mwenyekiti.
2 - Bi. Lilian M. Rugaitika -Mhariri Mkuu.
3 - Bi. Caroline H. Mulungu -Mhariri.
4 - Bi. Sauda N. Swai -Mhariri Msaidizi.
5 - Bi. Tusa D. Mwambenja -Msanifu wa Maudhui.

## KWA MAWASILIANO

Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA)
Kurasini -Makutano ya Barabara ya
kilwa/Nelson Mandela
S.L.P 9522
DAR ES SALAAM
Simu : +255 22 2851035-6
+255 22 2850717
+255 620 777 744
+255 677 777 746
+255 764 777 746
Baruapepe : tia@tia.ac.tz
Tovuti : www.tia.ac.tz
tiatanzania

TANZANIA INSTITUTE OF ACCOUNTANCY
TIA
"Education for Efficiency"